Yale ambayo wakulima wadogo wanaweza kufanya

6.1	Kuhusu viwango vya kimataifa vya kazi	33
6.2	Jinsi viwango hivi vya kazi vinavyoweza kukusaidia wewe binafsi na biashara yako	34
6.3	Utafaidika vipi kwa kufanya kazi na wanunuzi wako?	34
6.4	Yale ambayo wanunuzi wako huenda wakakutaka ufanye	34
6.5	Yale unayoweza kufanya sasa	35

KUCHUMA MBUNI, KITABU CHA PICHA, PICHA NA. 36

6

Yale ambayo wakulima wadogo wanaweza kufanya

Ikiwa wewe ni mkulima mdogo, sehemu hii inafafanua kile unachohitaji kufahamu kuhusu viwango vya kazi vya kimataifa na jinsi vinavyotekelezwa. Sehemu hii pia inapendekeza mambo unayoweza kufanya ili kuelewa au kuchukua hatua za kuinua hali za kazi katika shamba lako.

Sehemu hii imeandikwa kama hati zilizotengwa kwa wasomaji wanaotaka kuidondoa na kuinakili kwa mwanga ili kuisambaza kwa wakulima wadogo. Ikitumiwa kwa njia hii, inapaswa kuwa na vifungu vituafavyo vilivyoambatishwa kwayo:

- Kijitabu kiitwacho *Kufanya Kazi ili Kuboresha Maisha* **(zana za kufanyia kazi fungu F)**
- **Zana za kufanyia kazi fungu A:** (mfumo wa utekelezaji)
- **Zana za kufanyia kazi fungu E:** (sampuli za hati).

6.1 Kuhusu viwango vya kazi vya kimataifa

Ubora wa maisha yako ya kikazi ni muhimu kwa wengine na hata kwako wewe mwenyewe na familia yako. Mazao kutoka shamba lako yanauzwa katika nchi mbalimbali huko ng'ambo, ikiwa ni pamoja na Uingereza. Wateja wa Uingereza ni miongoni mwa wateja wengi ulimwenguni wanaoamini kuwa wafanya kazi wanaozalisha vyakula vyao wanapaswa kuwa na hali bora kazini.

Huenda ikawa tayari wateja wako washakueleza kuhusu viwango vya mahali pa kazi. Katika miaka michache ijayo wateja watatarajia utimize viwango vilivyoendelezwa awali na Shirika la Kimataifa la Wafanya kazi (ILO). Viwango hivi vya Shirika la Kimataifa la Wafanya Kazi (ILO) vimerekebishwa na shirika moja la Uingereza, liitwalo Ethical Trading Initiative (ETI) ili vitumiwe na makampuni ya Uingereza katika mitungo yao yote ya ugavi. (Mtungo wa ugavi unahusu watu na makampuni yote yanayohusika na kuchukua mazao kutoka mashambani na kuyapeleka hadi maduka makuu ya kujihudumia huko Uingereza. Kunaweza kuwa na hata watu sita katika mtungo huo baina ya mkulima na duka kuu la kujihudumia). Wateja na waajiriwa wao wa moja kwa moja pia wanafanya kazi ili kutimiza viwango hivi.

- Kwa muhtasari, viwango vya kazi vinavyotumiwa na ETI ni:
- Watu wanachagua ajiri wenyewe
- Uhuru wa kuungana na haki ya makubaliano ya pamoja zinaheshimiwa
- Hali za kikazi ni salama na safi
- Ajira ya watoto haitatumiwa
- Ujira unalipwa
- Masaa ya kazi hayazidishwi
- Hakuna ubaguzi wo wote unofanywa
- Ajira inayokubalika inatolewa
- Hakuna utendaji wa kikatili au usio wa huruma.

6.2 Jinsi viwango hivi vya kazi vinavyoweza kukusaidia wewe mwenyewe na biashara yako

- Kufanya kazi ili kutimiza hali bora zaidi za kikazi kutafaidi biashara yako kwa muda mrefu kwa Kusaidia mahusiano bora zaidi baina yako na wateja wako, kwa mfano, kwa kuhakikisha kwamba unaafikiana na masharti ya kazi yaliyo dhahiri;
- Kuinua ubora wa bidhaa na uzalishaji kwa kutumia vifaa vya kazi vyema zaidi, uwekaji wa kumbukumbu na kuratibu shughuli zako. Matokeo yake ni kwamba haya yatainua mapato ya shamba lako;
- Kuimarisha uhusiano mwema baina yako na wafanya kazi hivi kwamba visa vya kukosa kuja kazini vitapungua na hivyo uzalishaji utaongezeka;
- Kupunguza ajali na magonjwa yanayotokana na hali za kikazi pamoja na wakati unaopotezwa kutokana nayo;
- Kuimarisha heshima katika jamii yako;
- Kuleta biashara mpya kutoka kwa wafanya biashara wa soko la nje.

6.3 Je, kufanya kazi na wateja wako kunaweza kukusaidia vipi?

Wateja wengi tayari wana uzoefu wa kufanya kazi ili kutimiza viwango vya kazi vya kimataifa na unaweza kujifunza kutoka kwao. Wanaweza kukusaidia kuelewa majukumu ya hali za kazi ikiwa ni pamoja na wajibu wao kwenye mtungo wa ugavi, hadi kwa maduka makuu ya kujihudumia huko Uingereza. Hata hivyo, kitu muhimu wanachoweza kukupa ni ufahamu mkubwa zaidi wa utaratibu wote wa biashara ya soko la nje kutoka kwa shamba lako hadi kwa wateja wa mwisho wa mazao yako. Wanaweza kukupatia:

- Ufahamu bora zaidi wa soko na viwango unavyotakiwa kutimiza kwa ajili ya soko hilo. Kwa mfano, wateja wanaweza kutoa mafunzo au habari zaidi katika vituo vya ununuzi;
- Notisi ya mapema ya mabadiliko katika soko la mwisho la mtungo wa ugavi ili uweze kupanga kazi yako vyema zaidi;
- Nafasi ya kukueleza mtazamo wao kuhusu yale wanayohitaji kutoka kwako ili unufaike na ukulima wa kandokando;
- Fursa yako ya kuwaeleza yale unayohitaji kutoka kwao ili kuzalisha mazao yako ipasavyo;
- Msaada wa kiutendaji ili kuinua hali za kikazi. Kwa mfano, baadhi ya wateja wametoa bei bora zaidi kwa wakulima wadogo au uwezo wa kupata mkopo kwa urahisi kutokana na kuzingatia viwango hivi katika kazi yako.

6.4 Yale ambayo wateja wako watakutaka ufanye

Ikiwa wateja wako ndio wanaanza kufuata viwango vya kazi vya ETI, basi wanahitaji kuwa na habari za kuaminika kuhusu wakulima wadogo wote. Huenda wakatuma mtu kukagua shamba lako au wanaweza kukutaka ushiriki katika majadiliano kuhusu ya yale yanayohitajika kufanywa. Lengo la mazungumzo kama haya ni kugundua yale wewe unayofikiri kuwa ni masuala makuu ya mahali pa kazi. Unaweza kuhitajika kujibu maswali kuhusu shamba lako na kukutana na wakulima wengine ili mzungumze kuhusu masuala yenu muhimu kama kikundi. Kwa mfano, unaweza kuulizwa ni vipi kuwepo na mkataba ulioandikwa baina yako na mteja wako ni muhimu kwako.

Habari zitakazokusanywa kwa njia hizi zitamsaidia mteja kupanga atakayofanya baadaye. Orodha ya viwango vya kazi ni ndefu sana, na hakuna mtu anayetarajia wateja au wewe mwenyewe kushughulikia vyote mara moja. Mteja wako anapaswa kubuni mpango wa kushughulikia masuala yenu muhimu kwanza. Utaelezwa hatua zinazofuata. Hata hivyo, kumbuka kwamba haya yanaweza kuchukua muda mrefu sana.

6.5 Yale unayoweza kufanya sasa

Si lazima ungoje hadi mteja wako achukue hatua ya mwanzo. Unaweza kuanza kujifunza zaidi kuhusu viwango vya kazi na kuchukua hatua ukipenda:

- Soma kijitabu kiitwacho *Kufanya Kazi ili Kuboresha Maisha* kinachowasilisha mawazo makuu ya viwango vya kazi;
- Soma orodha yote ya viwango vya kazi angalia **zana za kufanyia kazi fungu A** ya hati hii. Hii haielezi tu viwango kwa ukamilifu, bali pia ina safu (katika rangi ya kijani kibichi) inayoonyesha unachoweza kufanya ili kutimiza kiwango hicho. Jua kwamba, katika mfumo wa utekelezaji 'mfanya kazi' inaweza kuwa na maana ya mtu ye yote anayefanya kazi katika shamba yaani wewe mwenyewe na familia yako, pamoja na wale unaowaajiri;
- Zungumzia familia yako na wakulima wengine wa kijijini umuhimu wa haya katika biashara zako;
- Zungumzia mashirika yo yote unayohusika nayo (kwa mfano chama chako cha ushirika au cha wafanya kazi) maana ya haya kwa biashara yako;
- Zungumzia wafanya kazi wako, ikiwa umeajiri ye yote, kuhusu masuala yao muhimu pale kazini. Huenda wakawa na ugumu wa kukueleza wazi hapo mwanzoni. Lakini kwa kuwauliza, unaonyesha kuwa unatamani kuwashughulikia na kuwafanyia biashara bora zaidi;
- Angalia sampuli za hati katika **zana za kufanyia kazi fungu E** zilizoandikiwa wakulima wadogo. Moja ya sampuli hizo ni mkataba baina ya mkulima mdogo na mteja, nyingine inapendekeza kumbukumbu unazoweza kuhifadhi na nyingine ni orodha ya kukagulia masuala husika ya afya na usalama. Unaweza kurekebisha hati mbili za kwanza ili zitumike katika shughuli za shamba lako. Orodha ya kukagulia masuala ya afya na usalama itakupa mawazo ya kuinua hali za kazi.

Ukishasoma usuli wote na kuzungumzia watu wengi unavyoweza, huenda ukataka kufikiria kuhusu vipaumbele vyako vikuu na kupanga yale yanayohitajika kufanywa kuviendeleza. Baadhi ya maendeleo huenda yakawa rahisi kutekeleza. Kwa mfano, unaweza kupata kwamba ni rahisi kuinua baadhi ya vipengele vya afya na usalama. Masuala mengine yatakuwa magumu zaidi kutekeleza. Hivyo, unapaswa kumuomba mteja wako akupe ushauri wa kutekeleza maendeleo hayo.